

# KARATASI YA KWELI KUHUSU KUSTAHIKI KWA WAHAMIAJI

Februari 2001

I. Wageni halali wanaweza kustahiki **pesa, ulezi wa watoto, na msaada wa kimatibabu (Medicaid na HealthWave)** ikiwa hao:

Wameishi nchini Marekani kabla ya Agosti 22, 1996 na wanafikia mojawapo ya masharti yafwatayo:

- Ni wakaazi halali wa kudumu
- Ni wakimbizi
- Ni watafuta stara
- Kufukuzwa kwao kumesitishwa
- Wamepewa kifungo cha nje
- Wamepewa hali maalum ya kuingia kwa masharti
- ni wazee waliotoka kiheshima au wanaotumika katika Huduma ya jeshi la Marekani (pamoja na mwenza na watoto ambao hawajaolewa wanaomtegemea mgeni huyo).
- wanaoingia kutoka Kuba au Haiti au kuchukuliwa kama wahamiaji wa Wahindi waamerika.

Waliingia Marekani baada ya Agosti 22, 1996 na wanafikia mojawapo ya masharti yafwatayo:

- ni wakimbizi
- ni watafuta stara
- kufukuzwa kwao kumesitishwa
- ni wazee waliotoka kiheshima au wanaotumika katika jeshi la Marekani
- Wageni halali wakaazi wa kudumu na wageni waliopewa kifungo cha nje au kuingia kwa masharti na hata pia wahamiaji waliochapwa na watoto wao hawastahiki msaada kwa miaka 5 kuanzia tarehe ya kuingia Marekani. Baadaye, ni lazima wafikie matoleo ya kuwa wageni ndiposa wapokee msaada.

Wageni wale wengine wote ambao hawaafikii vigezo vilivyopo hapo juu hawastahiki pesa, ulezi wa watoto, na msaada wa kimatibabu, lakini wanaweza kustahiki kugharamiwa matibabu ya dharura.

II. Wageni halali wanastahiki kuhusika katika mpango wa **Stampu za Chakula** kama ifwatavyo:

- A. Wageni wafwatao wanastahiki stampu za chakula kwa miaka saba tu kuanzia tarehe ya kuingia Marekani:
- wakimbizi
  - watafuta stara
  - wageni ambao kufukuzwa kwao kumesitishwa
  - Wanaoingia kutoka Kuba au Haiti
  - waliochukulia kama wahamiaji ambao ni Wahindi waamerika
- B. Wakaazi halali wa kudumu ambao wamefanyakazi kwota 40 za kustahiki (takriban miaka 10) au zaidi nchini Marekani au wale wanaopokea manufaa ya upofu au ulemavu na walikuwa na umri wa miaka 65 au zaidi mnamo agosti 22, 1996, au kwa sahi wako chini ya umri wa miaka 18.
- C. Mgeni ambaye anaishi kihalali nchini Marekani na aidha si mzee aliyetoka kiheshima au anayetumika katika huduma ya jeshi la Marekani. Hii ni pamoja na mwenza au watoto ambao hawajaolewa wanaomtegemea mgeni huyo.

III. Wageni halali wafwatao wanastahiki kipindi chote:

- A. Stampu za chakula na matibabu:
- Wahindi waamerika waliozaliwa Kanada
- B. Kwa ajili ya stampu za chakula:
- Washirika wa Kabila la Hmong au Lao wakati kabila hilo lilitoa msaada kwa watumishi wa Marekani wakati wa Enzi ya Vietnamu.

Wageni wale wengine wote ambao hawafikii vigezo vilivyopo hapo juu hawatastahiki manufaa ya stampu za chakula.

Kwa huduma zingine au kupata Ofisi ya Jamii na Urudishaji au Eneo la Kufikia lililo karibu na wewe, tumia viungo vilivyo mwisho wa ukurasa huu.

Ukurasa ulisasishwa mwisho: Septemba 16, 2004